# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA TISA

**09 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 09 FEBRUARI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS TAMISEMI:

**137. MHESHIMIWA BENARDETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha katika Shule za Msingi na Sekondari Mkoani Kagera.

**138. MHESHIMIWA ELIBARIKI EMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Mahaya - Singida.

**139. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa ajira za kutosha kwa Walimu ili kuondoa upungufu uliopo.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**140. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini baadhi ya miradi inayoibuliwa na Jamii kupitia TASAF hukataliwa na kutekelezwa miradi ambayo haikuibuliwa na Jamii.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

**141. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mikakati gani kuhakikisha changamoto za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi hazileti madhara nchini na lini zitapatiwa ufumbuzi.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**142. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Kata ya Oldonyosambu ambao Maeneo yao yalichukuliwa na Jeshi.

## WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**143. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLAH AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, ni kwa kiasi gani BAKITA na BAKIZA zinaondoa changamoto za matumizi ya Lugha ya Kiswahili Kitaaluma na Kijamii.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**144. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, mazungumzo kati ya Serikali na Mwekezaji wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa kuhusu Gesi Asilia ya Songosongo yamefikia hatua gani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**145. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, nini maandalizi ya Serikali kuhusu Teknolojia ya kutengeneza Watu wenye Akili Bandia na kulinda maadili ya Kitanzania.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**146. MHESHIMIWA MAULID SALEH ALI (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali imefikia hatua gani ya kuziunganisha na Mfumo wa NIDA Taasisi zote za Umma na Binafsi.

**WIZARA YA MAJI:**

**147. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji wa Vijiji 19 maarufu kama DAMBIA utaisha.

**148. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Bwawa la Mwanjoro litakarabatiwa ili kuwezesha usambazaji wa maji Vijiji vya Jinamo na Witamihya - Meatu.

**WIZARA YA NISHATI:**

**149. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itafunga laini ya pili ya umeme kutoka Geita hadi Sengerema ili kutatua tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara.

**150. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Rufiji zitalipwa fedha za CSR kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere.

## WIZARA YA KILIMO:

**151. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kufufua Skimu za Umwagiliaji za Ikindwa, Malolo na Nhalanga - Bukene ili zifanye kazi kwa tija.

**152. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje kuongeza tija kwenye Sekta ya Kilimo na kuimarisha soko la bidhaa.

**153. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaruhusu ushindani huru wa kibiashara kwenye Mazao ya Chai na Maziwa Wilayani Rungwe.

## WIZARA YA UJENZI:

**154. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Nyashimo - Ndutwa - Shigala - Malili hadi Ngasamo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**155. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaacha kuwafukuza na kuwavunjia vibanda Wajasiriamali wanaofanya biashara Barabara Kuu ya Segera – Korogwe - Moshi.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **09 FEBRUARI, 2024** | **KATIBU WA BUNGE** |